

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA)

Huu ni mpango wa Serikali wenye lengo la kuwawezesha wanyonge kumiliki uchumi wa nchi kupitia rasilimali na biashara wanazoendesha. Utekelezaji wa mradi huu unafanyika ili kusimamia na kuratibu shughuli za urasimishaji.

Pia kujenga uwezo wa urasimishaji biashara na uanzishwaji wa vituo vya biashara; Ardhi Mjini; ardhi Vijijini na kutoa elimu na habari kuhusu uwezesaji wa wananchi kupitia urasimishaji.

MKURABITA imekuwa na faida kwa wananchi kwani wameweza kurasimisha rasilimali na biashara wanazomiliki na kuzitumia kupata mitaji, mikopo na hatimae kuongeza kipato.

Faida nyingine ni iliyopatikana ni kuongezeka kwa pato la taifa kutokana na ongezeko la shughuli mbalimbali za uzalishaji mali; Kuongezeka kwa wigo wa walipa kodi na matumizi bora ya ardhi.

Pia umewezesha kuimarika kwa utawala bora kutokana na kuboresha mifumo ya kisheria na kitaasisi ambayo itarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na viwanda vidogo vya kusindika mazao kuanzishwa katika maeneo ya vijijini baada ya wakulima waliorasimishiwa ardhi kujengewa uwezo.